Tunza tangazo hili.
Onyesha tangazo kwa daktari au mtunzi.

Tiedote tuberkuloosista: swahili

# Tangazo kuhusu kifua kikuu na uchunguzi wa kifua kikuu

## Kwa sababu gani umepewa tangazo hili?

Watu waliyo na kifua kikuu Finland ni wachache. Kwa sababu ya utunzo mzuri imepotea karibu kabisa. Unafika kutoka nchi wapi wengi wanayo ugonjwa wa kifua kikuu. Unaweza kuwa na ugonjwa wa kifua kikuu na kuambukiza wengine karibu yako bila kujua. Kulingana na afya yako, afya ya ndugu zako na watu wengine karibu yako ni muhimu ya kwamba ugonjwa unayo fikiriwa kuwa kifua kikuu unagunduliwa na kutunzwa mapema.

Finland inataka kutunza afya ya wahamiaji. Kwa sababu umefikiria kuwa Finland kwa zaidi ya miezi mitatu una haki ya kuenda kwenye picha ya mapafu/eksirei kwa bure. Kuenda kwenye picha ni ya huru. Pamoja na picha ya mapafu inachunguliwa kama unayo mabadiliko ya kifua kikuu kwenye mapafu yako.

## Picha ya mapafu/eksirei

Kifua kikuu cha mapafu inagunduliwa kawaida kupitia picha ya mapafu. Kuchukua picha ni salama. Aliye na ujauzito anastahili kusema kuhusu hali yake kabla ya kuchukuliwa picha. Mwanamke nani hana dalili anachukuliwa picha miezi za mwisho karibu kujifungua.

Picha ya mapafu inachukuliwa kwenye kituo cha afya cha mji wapi unaishi. Picha ya mapafu ni bure kwako. Kama kwenye picha ya mapafu kuna utofauti utapangwa muda wa kuenda kwenye uchunguzi ya kuona zaidi.

Ujiandikishe kwenye picha ya mapafu haraka iwezekanavyo!

Onyesha tangazo hili kwa mtunzi wa kituo cha afya/mtunzi wa mahali pa picha za mapafu (röntgen).

Habari za kuwasiliana na kituo cha afya/mahali pa picha za mapafu (röntgen): ______________________

______________________________________________________________________

## Dalili za kifua kikuu ni za aina gani?

Dalili muhimu za kifua kikuu za mapafu ni kikohozi kilicho endelea kwa zaidi ya wiki tatu inayo weza kubadilika baadaye kuwa na makamasi. Wakati wa kukohoa sana makamasi inaweza kuwa na rangi ya anjano, rangi ya udongo au na damu. Ugonjwa ukiendelea mtu ataweza kusikia shida ya kupumua na maumivu ya kifua.

Mtu aliye na kifua kikuu anaweza kuwa na homa, kukonda au kutoa jasho jingi wakati wa usiku. Inawezekana anakosa hamu ya chakula na nguvu zake kupungua. Dalili zinaweza kuwa zingine pia kulingana na mahali ya ugonjwa mwilini.

Kwa watoto kifua kikuu inasababisha ukuaji na maendeleo yao kuanza kuenda polepole.

## Unafanya nini ukiwa sasa na dalili zinazo faa kifua kikuu au zinaonekana baadaye?

Wasiliana bila kuchelewa na kituo cha afya cha mji unapoishi. Uchunguzi unayo fanywa na daktari ni ya lazima. Uchunguzi unayo fanywa na daktari ni ya bure kwako. Taarifa kuhusu uchunguzi hautafika kwenye taarifa walizonazo na Waafisa ya Uhamiaji (*maahanmuuttoviranomainen*).

## Kifua kikuu ni nini?

Kifua kikuu sio sababu ya mtu yeyote. Kifua kikuu ni ugonjwa wa kuambukizwa. Ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria inayoitwa *Mycobacterium tuberculosis*. Kama kawaida kifua kikuu iko kwenye mapafu wapi itakuwepo eneo iliyo ambukizwa na mabakteria. Kutoka hapo mabakteria yanaweza kuzambaa kupitia damu au limfu kwenye eneo zingine za mwili kwa mfano kinindu za limfu, utumbo, ngozi au mfumo mkuu wa fahamu. Kifua kikuu inaweza kuwa kwenye mapafu na hapo papo pia pengine mwilini.

## Namna gani kifua kikuu inaambukizwa?

Kifua kikuu huenea kwa njia ya hewa kutoka mtu moja kwa mwingine. Mtu aliye na kifua kikuu akiongea, akiimba, akikohoa au kupiga chafya mabakteria ya kifua kikuu yanaingia hewani. Hapo mtu aliye kwenye chumba kile anaweza kupata mabakteria kwenye mapafu zake kupitia hewa aliyovuta. Hapo wale waliyo pamoja na mgonjwa kwa muda mrefu wanaweza kupata ugonjwa. Hali ya kijuu cha kuambukizwa ni kwa watu wa familia wanayo ishi pamoja.

## Nani anapata ugonjwa wa kifua kikuu?

Mtu moja tu kutoka kumi waliyo ambukizwa na kifua kikuu wanapata ugonjwa wa kifua kikuu. Wanayo weza kupata ugonjwa kwa urahisi ni watoto wadogo chini ya umri wa miaka 5, vijana, wazee na watu nani mwili wao haina nguvu ya kukinga.

## Inachukua muda gani kabla kiambukizi cha kifua kikuu inabadilika kuwa ugonjwa wa kifua kikuu?

Mtoto mdogo chini ya umri wa miaka 5 nani hajapata nchanjo anaweza kupata ugonjwa hata chini wa wiki au miezi michache na ugonjwa unaweza kuzambaa haraka. Mtu mkubwa nani hana magonjwa za kawaida anapata ugonjwa kama kawaida baada ya mwaka moja, miaka miwili kutoka wakati alipoambukizwa. Mtu anaweza kupata ugonjwa wa kifua kikuu hata baada ya miaka kumi na zaidi kutoka wakati wa kuambukizwa. Kwa hivyo kumbuka dalili za kifua kikuu.

## Kifua kikuu inachunguliwa (vipimo na uchunguzi) wapi na vipi?

Uchunguzi unaanza kwenye kituo cha afya, kwenye utunzo wa afya ya wanafunzi au ya wafanyakazi. Uchunguzi zaidi unafanywa hospitalini. Watoto wanapimwa kwenye wadi au polikliniki ya magonjwa ya watoto. Kifua kikuu cha mtu mkubwa unachunguliwa na kutibiwa hospitalini kwenye wadi au polikliniki ya magonjwa ya mapafu.

Kama inafikiriwa mtu amepata kifua kikuu picha ya mapafu inachukuliwa na sampuli ya kikohozi inachunguliwa. Kutoka sampuli ya kikohozi inafanywa kupakwa rangi na kupanda kifua kikuu. Ikihitajikwa kutoka kikohozi inaweza kuchukuliwa kipimo cha haraka kuonyesha kama mtu anaye ya kusababisha kifua kikuu.

Mara nyingine kuna haja ya kuchungulia koromeo kwa kindani na mpira au kuchukua picha ya ukamilifu zaidi ya mapafu (kerroskuvaus). Wakati wa kuchungulia kifua kikuu kutoka pengine kasoro mapafu namna mbali mbali za kuchukua picha zinatumiwa. Zaidi ya hapo inajaribiwa kuchukua sampuli ndogo kutoka mkusanyiko wa seli au ya usaha.

## Namna gani kifua kikuu inatunziwa (matibabu)?

Kifua kikuu inatunziwa na madawa. Mwanzoni madawa yapo angalao nne. Kutunza kifua kikuu cha kawaida inachukua angalau nusu mwaka. Mtu anapona vizuri kutoka kifua kikuu kama kifua kikuu inagunduliwa mapema na utunzo unawezekana kulingana na muda unayo hitajikwa. Utunzo wa kifua kikuu Finland ni nzuri na ni ya bure.

Soma zaidi kuhusu kifua kikuu: [www.tuberkuloosi.fi](http://www.tuberkuloosi.fi)